

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA RUKWA

Telegraphic: "REGCOM"

Simu. No:0252802137/2802138/2802144

Fax No. (025) 2802217/2802318

E-mail:ras.rukwa@tamisemi.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA,
P. O. Box 128,
SUMBAWANGA.

03 Aprili, 2017

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI RUKWA

Ninayo mambo mawili muhimu nataka kusema kwa Wananchi wa Mkoa wa Rukwa.

Kwanza, ni mkutano niliohudhuria mwishoni mwa mwezi Machi, huko Lusaka nchini Zambia. Nilipata mwaliko wa 361 Degrees Africa baada ya kupewa kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkutano huo ulihusu kupitia na kuhamasisha biashara kati ya Tanzania na Zambia ambayo hatimaye lengo lake ni kuboresha mazingira kibiashara.

Lakini vile vile kupanua wigo wa fursa za kibiashara na kiuchumi kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zambia. Mkutano huo ulifunguliwa na Balozi wa Tanzania nchini Zambia Mheshimiwa Grace Joan Mujuma. Mkutano huu uliwashirikisha pia wadau mbalimbali toka upande wetu wa Tanzania na Zambia. Lakini kwa kifupi jambo nililoliona

ni kwamba Mkoa wa Rukwa unapakana na Nchi ya Zambia kwa upande wa Kusini Magharibi mwa Tanzania na tuna mipaka ya Kasesya na Mosi ambayo inaweza kuwa ya manufaa kwa nchi hizi mbili.

Hali kadhalika tuna Bandari ya Kasanga ambayo vyombo vya usafiri wa majini hutumika mpaka nchini Zambia. Kuwepo kwa mipaka hiyo hurahisisha mawasiliano ya Biashara kati ya Zambia na Tanzania. Hivi sasa barabara ya lami kutuunganisha na Bandari ya Kasanga ipo katika hatua za mwisho kukamilika na Barabara ya Matai – Kasesha ipo katika mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Mkoa wa Rukwa ni moja kati ya mikoa inayozalisha mazao ya chakula na biashara.

Hali kadhalika tuna mifugo na samaki. Baadhi ya wadau wa biashara nchini Zambia wameonesha mahitaji yao makubwa kwenye mchele, maharage, alizeti, viazi na samaki wa kukaushwa kwa moshi.

Ningependa nitoe wito kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa kuona umuhimu wa kutumia fursa hii kwa kujiunga katika vikundi au ushirika ili kuweza kuboresha uzalishaji na kuongeza mnyororo wa thamani ili kushika soko hilo kwani ni karibu kuliko kutafuta masoko ya mbali. Jambo la muhimu ni kuzingatia suala la ubora na ufungashaji. Mambo hayo yakiwepo katika kiwango kinachostahili itafungua na fursa zingine mfano usafirishaji na kadhalika.

Ningependa Halmashauri katika Mkoa huu ziwajengee uwezo wakulima wetu na wafanyabiashara ili kuingia katika ushindani wa kibiashara na wenzetu.

Kwa kuwa tupo katika juhudi za kuhakikisha viwanda vinaanzishwa katika Wilaya zetu natoa wito Wilaya zote zihakikishe zinatengeneza mazingira ya kuwa na viwanda vya uchakataji ili kuepuka kuuza mazao yetu ambayo hayajaongezwa thamani. Lakini pia nawakaribisha wawezekaji wa nje kwa kuwa tunayo ardhi ya kutosha kujenga viwanda katika Mkoa wetu.

Tutajitahidi kupitia ujirani mwema na kwa kushirikiana na 361 Degrees Africa ambao wameonesha nia ya dhati kutengeneza mazingira ya biashara na jirani zetu wa Zambia.

Jambo la pili, tunategemea kupokea Mwenge wa Uhuru 07 Aprili, 2017 kutoka Mkoa wa Katavi katika kijiji cha Kizi Wilayani Nkasi. Mara baada ya mwenge kupokelewa utakimbizwa katika Wilaya zote Tatu na Halmashauri zake. Ni mategemeo yangu kwamba wananchi katika Wilaya zote katika maeneo yote utakapopita watajitokeza kwa wingi kwenye shughuli zote ambazo zitapitiwa na Mwenge wa Uhuru pamoja na kuwaona wakimbiza Mwenge wa Uhuru wa Kitaifa kwa mwaka 2017.

Katika mbio hizo kutakuwa na shughuli za kuweka mawe ya msingi, uzinduzi wa miradi iliyokamilika na kusikia ujumbe wa Mbio za Mwenge kutoka kwa Wakimbiza Mwenge na mikesha. Na hatimaye mnamo tarehe

11 Aprili, 2017 Mwenge wa Uhuru tutaukabidhi kwa jirani zetu wa Mkoa wa Songwe katika kijiji cha Mkutano.

Natumaini wananchi wote wa Mkoa wa Rukwa wanaelewa na kuthamini Mbio hizo na natumaini wote tutajumuika na kuona Mkoa wetu unakuwa mstari wa mbele kuenzi mbio hizo. Natoa wito kwa viongozi ngazi ya Wilaya na Halmashauri kuwapa nafasi ya kutosha wananchi kushiriki katika mbio hizo.

Zelote Stephen Zelote

MKUU WA MKOA RUKWA